

102/3
KISWAHILI
FASIHI
KARATASI YA TATU
MUDA: SAA 2.30

MITIHANI WA PAMOJA WA SUNSHINE NA PANGANI
SUPAJET, JULAI 2013

MAGIZO

1. Umepewa maswali saba. Jibu maswali manne pekee.
2. Swali la kwanza ni la lazima
3. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.
4. Chagua swali moja moja kutoka kwa kila sehemu zilizosalia.

SEHEMU	UPEO	TUZO
A.TAMTHILIA	20	
B.RIWAYA	20	
C.HADITHI FUPI	20	
D.USHAIRI	20	
E.FASIHI SIMULIZI	20	
JUMLA	80	

SEHEMU A: TAMTHILIA - 'MSIWAHIKI MEYA' – Timothy Arege

(ALAMA 20)

1. Fafanua namna asasi na vikundi vifauatavyo vinavyochangia kuendeleza maovu dhidi ya umma wa Cheneo huku ukirejelea tamathilia husika.
 - a) Idara ya polisi
 - b) Dini
 - c) Nchi za magharibi
 - d) Kamati za Baraza

SEHEMU B: RIWAYA - 'UTENGANO' – Said A. Mohammed

2. "Ukombozi wa mwanamke uko mikononi mwake mwenyewe". Kwa kurejelea riwaya ya 'Utengano' thibitisa ukweli wa dhana hii. (alama 20)
3. (i) Kimya kingine. Miguu tu ndio iiyokuwa ikichuana na njia. Wakaendelea na safari yao.
 - a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
 - b) Fafanua mbinu moja ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. (alama 2)
 - c) Eleza sifa tano za mmoja wa wahusika katika dondoo hili. (alama 10)
- (ii) Fafanua ujumbe uliomo katika barua aliyotumia Said A Mohamed katika riwaya. (alama 4)

SEHEMU C - HADITHI FUPI – DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE

Walialila, K na S.A Mohamed.

4. a) Anwani 'Kanda la Usufi' inafiki hadithi husika. Thibitisha (alama 10)
 - b) Dhihirisha matumizi ya kinaya katika hadithi ya 'Tazamana na Mauti.' (alama 10)
5. (i) "Salaaala, mbona wasirudi kwao waishi maisha ya maana."
 - (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
 - (b) Mnenaji ana umuhimu gani katika hadithi hii? Toa hoja mbili (alama 4)
- (ii) Jadili matumizi ya mbinu rejeshi katika hadithi zozote tatu katika diwani ya "Damu Nyeusi" (alama 12)

SEHEMU D : USHAIRI

(alama 20)

Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.

Nimeyaandika maneno haya
kwa niaba ya,
Mamilioni wasio mavazi
Wazungukao barabarani bila mavazi
Wabebao vifurushi vilivyo wazi,
... milki yao ya maisha.

Kwa niaba ya:
Maelfu wanaovuma bila haki
Wiki baada ya wiki
Leo sumu au spaki
Leo kamba au bunduki
Na kwa wale wanasubiri kunyongwa

Kwa niaba ya
Vijana walio mtaani
Wale mayatima na maskini
Wazungukao mapipani
Kila pembe mjini
Kuokota sumu kutia tumboni
Kujua bila kujua
'ili kupata kuishi.

Kwa niaba ya:
Wakongwe wasiojiweza
Walao chakula kilichooza
Wachukua choo wakijipakaza
Pole pole wakijiangamiza
Katika vyumba vyao
Baridi na giza
Kwa saba hawan watazama
Wala wauguza

Kwa niaba ya:
Waishi na nyingi hofu
Kw sababu ya madawa tifutifu
Yatiwayo vyakulani yakitufanya wafu
Bila ya mtu kuona
Kana kwamba sote to vipofu

Kwa niaba yetu sote:
Tuliofungwa vifunguni, duniani
Tuliosukumwa kingoni, maishani
Tuliopokonywa maoni machoni
Tulioitiwa sumu malishoni
Tuliodidimizwa kinyesini

Ili 'maendeleo'
Yaendeleee kwenda njiani
Huku yakitema machicha ya roho zetu.

Maswali

- 1) Hili ni shairi la aina gani? (alama 2)
- 2) Eleza matatizo yanayokumba wanaorejelewa katika shairi? (alama 6)
- 3) Eleza maana ya mishata na utambue mfano mmoja katika shairi. (alama 2)
- 4) Malenga ametumia idhini yake. Jadili kwa mifano miwilli. (alama 4)
- 5) Kwa kutoa mfano mmoja, eleza mtindo aliotumuia mshairi kuendelea ujumbe wake. (alama 2)
- 6) Andika ubeti wa kwanza kwa lugha nathari/tutumbi (alama 4)

7. SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI (alama 20)

- a) Eleza matatizo matano yanayoweza kuikabili fasihi simulizi katika jamii. (alama 10)
- b) Taja na ueleze wahusika wanne wa fasihi simulizi (alama 4)
- c) Tofautisha kati ya ngonjera za ushairi na za maigizo (alama 2)
- d) Fafanua vipera vifuatayo vya fasihi simulizi (alama 4)
 - (i) ngoma
 - (ii) ngomezi